MOSHI CO-OPERATIVE UNIVERSITY (MoCU)
CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI

Sokoine Road,
P.O. Box 474,
Moshi, Tanzania.
Tel:+255 272754401
Fax:+255 272750806
e-mail: info@mocu.ac.tz
Website: www.mocu.ac.tz

OFFICE OF THE VICE CHANCELLOR
P.O. Box 474,
Moshi, Tanzania.
Tel: +255 27 2751833
Fax: +255 27 2750806
E-mail:vc@mocu.ac.tz

# TAARIFA KWA UMMA



## NDUGU. GEORGE D.YAMBESI

## UTEUZI WA MWENYEKITI WA BARAZA LA CHUO NA MANAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO

Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), inapenda kutoa taarifa kwa umma kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, amemteua ndugu George D. Yambesi (pichani) kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Baraza la Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) kuanzia tarehe 24 Januari, 2018.

Mkuu wa Chuo Mhe. Pius Msekwa alimtambulisha Mwenyekiti huyo alipokutana na wafanyakazi wa Chuo

Kikuu cha Ushirika Moshi tarehe 05 Machi, 2018 katika Ukumbi wa George Kahama Chuoni hapo na kumtakia kazi njema katika jukumu hilo jipya la kukijenga Chuo. Ndugu George Yambesi ni Katibu Mkuu mstaafu.

Aidha, kwa mamlaka aliyonayo Mkuu wa Chuo amemteua Prof. Alfred Said Sife (PhD), kuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma) na Prof. Fredy Timothy Mlyavidoga Kilima (PhD), kuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Utawala na Fedha) kwa kipindi cha miaka minne (4). Uteuzi huu umeanza rasmi tarehe 01 Machi, 2018. Kabla ya kuteuliwa kwao Prof. Alfred Said Sife (PhD) na Prof. Fredy Timothy Mlyavidoga Kilima (PhD) walikuwa watumishi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).



**Prof. Alfred S. Sife (PhD)**



**Prof. Fredy T. M. Kilima (PhD)**

Prof. Alfred Said Sife na Prof. Fredy Timothy Kilima pia walitambulishwa kwa wafanyakazi katika hafla hiyo iliyofanyika hapo Chuoni tarehe 05 Machi 2018.

## IMETOLEWA NA MENEJIMENTI YA MoCU